REPOA wabaini changamoto sekta za gesi, mafuta

Na Glory Mhiliwa

KUGUNDULIWA kwa mafuta Kusini kwa Tanzania imeelezwa kuwa ni kichocheo kikubwa katika ukuaji wa uchumi sambamba na kuongezeka ajira.

Sekta hiyo inahusisha maelfu ya ajira sambamba na kuongezeka kwa mapato ya sekta za afya, miundombinu, elimu pamoja na kwa hiyo nchi itakuwa na fedha kwa kukujipatia mapato yatokanayo na mafuta.

Mara baada ya kusainiwa kwa sheria ya mafuta na Rais Desemba 2015 baada ya kupitishwa na Bunge Julai 2015, Kituo cha utafiti cha REPOA, kilifanya utafiti katika sekta hiyo ili kupata maoni kutoka kwa wadau ambapo Ubalozi wa Norway hapa nchini ndio uliofadhili utafiti huo.

Matokep ya utafiti huo yalibainisha kuwa ushirikishwaji wa wananchi kuhusiana na gesi ndio suluhisho pekee la mafanikio ya sekta hiyo.

Wakati wa kukusanya maoni, REPOA iliyahoji makampuni ya kimataifa ya mafuta yanayoendesha shughuli zake hapa nchini,Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC),wafadhili wenye nia katika sekta hiyo,Taasisi za elimu pamoja na taasisi zisizo za Kiserikali (NGOis).

Mkurugenzi wa mikakati na tafiti wa REPOA, Abel Kinyondo ambae ndiye aliyeongoza utafiti huo, anaelezea matokeo ya tafiti huo ambapo anasema licha ya nchi kupitisha sera na sheria za kuwawezesha wananchi wa hali ya chini wanufaike na sekta hiyo lakini ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kuwa inasimamia ili wananchi hao waweze kunufaika.

"Hakuna sera wala sheria yoyote kwenye sekta hii inapozungumzia wajibu wa serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wa chini wananufaika na mafuta, tukiangalia nchi kama Nigeria au Angola sera na sheria zao zinafanana na ya hapa nchini," anasema.

Anasema lakini hapa nchini wanaonufaika na sekta hiyo ni wachache ambao ni matajiri na siyo wananchi wa hali ya chini ambao mtaji kwao ni mdogo.

Anatoa mapendekezo ambayo wadau waliyatoa wakati wa utafiti ambayo,kwamba serikali inapaswa kuyachukua ili kuhakikisha kuwa sekta hiyo inakuwa na tija kwa wote hususani wa kipato cha chini.

Anasema, kwanza wajibu wa Serikali katika kuwasimamia na kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini kunufaika na sekta hiyo ujulikane kisheria ambapo hadi hivi sasa hakuna sera wala sheria ya sekta hiyo inayozungumzia wajibu wowote wa Serikali katika kuwasaidia wananchi hao.

Aidha Serikali inawasaidiaje wananchi wa nyanja zote kama wakulima kwa kuhakikisha inawapatia wataalamu wa zao husika kuwapatia pembejeo na kuwaelimisha namna ya kulima ili kilimo cha kisasa mazao yao yawe na ubora wa kimataifa.

Anasema kwa kufanya hivyo itasaidia mazao ya wakulima kupata soko ambapo fedha za kusimamia miradi hiyo inatoka kwenye mafuta.

Aidha anabainisha kuwa sera ya Taifa ya mwaka 2013ya uwekezaji kwenye manunuzi ya bidhaa inazitaka kampuni zinazowekeza hapa nchini kwenye sekta hiyo kufanya manunuzi ya bidhaa zao hapa nchini.

Lakini kwa kufuata ubora unaotakiwa hivyo bila ya Serikali kuwasaidia wananchi wa chini kuzalisha bidhaa zenye ubora hawataweza kupata soko la bidhaa na mazao yao kwa kuwa hayana ubora unaotambulika kimataifa.

Anasema kuwa makampuni katika sekta ya mafuta, ni kampuni kubwa zenye wafanyakazi wengi hivyo ili wananchi wa hali ya chini waweze kufanikiwa kupata masoko ya bidhaa zao moja kwa moja ni lazima Serikali iwaunganishe wananchi hao nchi nzima.

Kinyondo anasema kuwa kapuni zinazojishughulisha na uchimbaji na utafiti wa mafuta ni kampuni kubwa zenye wafanyakazi wengi hivyo bidhaa ambazo zitahitajika ni nyingi na zenye ubora.

Anasema Serikali ikifanya hivyo wananchi wa kipato cha chini ndio wataweza kunufaika na sekta hiyo kinyume na hapo wanufaika watakuwa ni wale wote wenye mitaji mikubwa ambao wataliteka soko hilo kutokana na kuwa na mtaji.

Aidha anasema Serikali ndio ifanye ushirikishaji wa wananchi siyo wananchi ndio wajishirikishe ambapo Serikali inapaswa kuwa na sera ndogo nzuri itakayosimamia upatikanaji wa mapato kwenye mafuta ili iweze kuwanufaisha

> *Hakuna sera wala sheria yoyote kwenye sekta hii inapozungumzia wajibu wa serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wa chini wananufaika na mafuta, tukiangalia nchi kama Nigeria au Angola sera na sheria zao zinafanana na ya hapa nchini ...*
>
> **Abel Kinyondo.**
> Mkurugenzi wa Mikakati na Tafiti REPOA




Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Madimba, Mtwara hadi Dar es Salaam.

wananchi kupitia miradi mbaimbali ya kiamendeleo.

Anasema Serikali ianze utambuzi wa wataalamu wa mafuta walioko hapa nchini ambapo japokuwa bado shughuli za uchimbaji hazijaanza lakini inapaswa kufahamu uhitaji wa wenye sifa katika sekta hiyo na wataalamu walipo kwa kushirikiana na taasisi za ndani.

"Nchi ya Norway ni kati ya nchi iliyofanikiwa sana kimaendeleo kwa kuitumia vyema sekta hii ambapo, kwao mafuta yaligundulika 1940, lakini walianza kuchimba mwaka 1970; hiyo miaka thelathini waliitumia katika kujiandaa kwa kuwajengea uwezo wananchi wake ili sekta hiyo iendeshwa na wazawa wenyewe," anasema Kinyondo.

Anasema Norway imeweza kufanikiwa kutokana na kuwa na sera mbalimbali ambazo toka awali ziliwashirikisha wananchi na zimelenga kuhakikisha kuwa wanufaikaji walengwa wa sekta hiyo ni wananorway.

Katika sera hizo zimewezesha Serikali kutoa mafunzo kwa kampuni za kihandisi za nchini humo ili ziweze kuendesha sekta hiyo kupiga hatua katika sekta za elimu afya na miundombinu kupitia mafuta.

Ripoti hiyo inapendekeza kuwa iwapo Serikali itakuwa na umiliki kwenye mafuta itasaidia kuondoa kampuni hewa.

Anasema kampuni yoyote itakayokuwa inajiendesha kwenye sekta hiyo ni lazima iwe imesajiliwa hapa nchini na watanzania wawe na hisa.

"Kupitia umiliki wa Serikali kwa kuwa na hisa badala ya kutegemea mapato kutokana na kodi , itasaidia sana kwenye kuongeza mapato na hata suala la usimamizi itakuwa ni rahisi zaidi kama Botswana kwenye sekta ya madini wamepiga hatua kubwa ni kutokana na Serkali kuwa na umiliki wa kampuni za uchimbaji madini," anasema Kinyondo.

Pia Serikali iwashirikishe wananchi katika kupata maoni ambapo zoezi hilo liendeshwe kwa uwazi kwa kushirikisha wadau wote ambapo kupitia ushirikishwaji.

Aidha utafiti huo ulipendekeza kuwepo na sheria na taratibu nzuri zitakazowezesha kupatikana kwa suluhisho dhidi ya changamoto zilizotolewa.

Mpaka sasa mataifa makubwa ambayo tayari yameshaonyesha nia ya kuwekeza kwenye sekta ya mafuta hapa nchini ni Umoja wa Ulaya,Marekani, Uingereza,Denmark pamoja na Norway.